

PASIANSI WILDLIFE SECURITY COMPANY LIMITED – PASCO



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA ULINZI (SECURITY GUARDS) 100

Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi – Mwanza imeanzisha Kampuni binafsi ya Ulinzi yenyenye namba ya usajili 143836754. Majukumu makuu ya kampuni hii ni kufanya kazi ya ulinzi katika Hoteli, Loji, Kambi za Utalii na Ofisi za Serikali na maeneo binafsi.

1. MAJUKUMU YA KAZI ZA WALINZI (SECURITY GUARDS)

- Kuhakikisha usalama wa watu na mali zilizopo eneo la kazi
- Kuzuia vitendo vya uhalifu sehemu ya kazi
- Kusindikiza misafara ya watalii ndani na nje ya maeneo ya hifadhi
- Kuzuia wizi na majanga ya moto eneo la kazi
- Kufanya doria eneo atakalopangiwa
- Kusimamia eneo la kupaki magari lililopo eneo la kazi
- Kutoa huduma nzuri kwa mteja eneo la kazi
- Pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na uongozi

2. VIGEZO VYA KUZINGATIA

- Awe ni raia wa Tanzania kwa uthibitisho wa cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha taifa au hati ya kusafiria
- Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi
- Awe na elimu ya Uhifadhi wa Wanyamapori au Utalii kuanzia ngazi ya cheti cha awali kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali
- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 35
- Kwa mwombaji mwanaume awe na urefu kuanzia futi 5'6 na mwanamke 5'0 na kuendelea
- Awe na uwezo wa kusoma, kuandika na kuongea kwa ufasaha lugha za kiswahili na kiingereza. Ujuzi wa lugha za kifaransa, kihispania, kichina, etc. ni sifa za ziada

- Asiwe na tuhuma yoyote Mahakamani au kuwahi kuhukumiwa kwa kosa la jinai
- Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atakayopangiwa
- Awe na afya njema (utimamu wa mwili)
- Asiwe na michoro (tattoo) yoyote katika mwili wake

3. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Maombi yatumwe yakiambatana na vifuatavyo;

- Wasifu wa mwombaji
- Nakala za vyeti vya elimu vilivyothibitishwa na Mwanasheria
- Picha ndogo nne (passport) na picha kamili (full size)
- Majina na anuani za wadhamini watatu

4. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27 Mei 2022, saa 9:30 mchana.

Yatumwe kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI,

PASIANSI WILDLIFE SECURITY COMPANY LIMITED,

P.O BOX 1432,

MWANZA.

Simu: +255 282 560 333

Barua pepe: principal@pasiansiwildlife.ac.tz

Tovuti: www.pasiansiwildlife.ac.tz